Soma hii tafadhali……

# YUKO WAPI?

Ilikuwa ni mida ya jioni, ambapo jua lilishaanza kutokomea upande wa magharibi. Mawingu machache tu ya rangi ya kijivu yalikuwa yamebakia bakia kwenye anga lililoshageuka kuwa jekundu sana.

Nikiwa juu ya ghorofa refu kabisa lenye takribani floor thelathini na moja ndani ya jiji la Daar es alaam. Nililiona vizuri mno namna anga lilivyokuwa kutokea hapo juu. Hata ndege nao walionekana wakirejea kutoka kwenye mizunguko yao.

“Is it a time to die, right now?”, iliniuliza nafsi yangu, ambayo ilinishuhudia nikiwa nimesimama kuelekea ukingoni kabisa mwa ghorofa hilo.

Lilikuwa ni ghorofa refu mno ndani ya jiji hilo la kibiashara.

Basi nilipotazama chini, kwa mbali sana niliweza kuyaona magari yakikatiza na kupishana katika moja ya makutano ya barabara hizo za hapo mjini. Pia watu walionekana wadogo! Kama sisimizi wakiingia na kutoka mitaa mbalimbali.

FREE SAMPLE

Baada ya kutembea na kufika kwenye tofali la mwisho kabisa ukingoni. Ndipo nikafumba macho yangu.

“Are you going to do it?”, nafsi yangu iliendelea kuniuliza.

Upepo mkali mno uliendelea kunipuliza huku nikiwa nimefumba macho na shati nililolivaa lilipeperuka kama bendera iliyokuwa ikinadi chama fulani. Mbele yangu ilikuwepo drone iliyosetiwa kuweza kurekodi kila hatua na kitu nilichokuwa nakifanya.

Nilikuwa nimeshaiset moja kwa moja na kuruka live kupitia social networks na baadhi ya websites. Kwa hiyo kila nilichokuwa nakifanya kuna baadhi ya watu waliokuwa waki-stream online na kutazama.

Upande wa mbele ya ghorofa nililopo kulikuwa na ghorofa jingine lililokuwa na bango kubwa sana. Bango lililoonesha tangazo la juisi tamu kabisa itokanayo na zabibu.

“Won’t you miss the Grapes?”, nafsi yangu iliendelea kuniuliza.

FREE SAMPLE

"Yes, I will miss the Grapes. But jamii haitani-miss mimi, And so… I have to die". Nilisema huku nikipeleka mkono usoni kuweza kuivua mask iliyonificha sura yangu halisi.

Sasa nilitaka kujiweka wazi kwamba mimi ni nani?. Na kisha kujiua kwa kujirusha kutoka juu kabisa kwenye hilo ghorofa refu mno.

Nilipoishika mask  na kutaka kuivua…

"But Why?", nafsi yangu iliniuliza.

Hapo kila mmoja aliyekuwa anashuhudia kwa kutazama video ile alibaki kunihuzunikia. Kila mtu alibaki kimya akitafakari kuhusu nini kilichonipelekea kutaka kufanya hiki ninachokifanya. Wengine mioyo yao ilidunda kwa kasi mno kwa kuhofia mauaji yatakayoenda kutokea hivi punde.

Online viewers wakiwa zaidi ya laki moja kutoka sehemu mbalimbali za Afrika na nje ya Afrika pia, walikuwa wakishuhudia na kutazama tukio hilo.

"Think about it in another way", Nafsi ilisema tena.

FREE SAMPLE

“Noo!”, nilikataa na kuikataza nafsi. Na kisha nikasema,

“There is no way but one way. And that is, I HAVE TO DIE!”.

Basi nikiwa nabishana na nafsi yangu, mara ghafla kitu kizito kiliweza kunisukuma na kunidondosha kutoka juu kabisa ya ghorofa lile.

“What happened!”, nilibaki najiuliza.

Nikiwa nateremka sasa kwa mbali nilikiona kifo kikijiandaa kunipokea kwa mikono miwili.

Hapo tena, ni woga na wasiwasi vikaanza kunitawala. Nilijikuta ghafla sitaki tena kufa. Nilijikuta naanza kuyatamani tena maisha kwa kutaka kuipata nafasi nyingine ya kuweza kuendelea kubaki hai duniani.

“Are you regretting now?”, mara nilisikia nafsi yangu ikiniambia na kuniuliza kama najutia kwa maamuzi niliyoyafanya?. Kumbuka hapo nikiwa hewani nashuka kuelekea chini ardhini.

FREE SAMPLE

“Shut up!”, niliijibu kwa hasira na kuikaripia mno. Kisha nilituliza mzuka na kuiambia tena kwa upole.

“I WANT TO REMAIN ALIVE!. Hivi huoni kuwa bado nakuhitaji wewe?. Nayahitaji maisha yangu pia”

Oh shit!, ndipo nilipoanza kujibinua binua hewani nikijaribu kutafuta namna ya kuutetea uhai wangu.

“Ni nini hiki?”, nilijiuliza mara baada ya kupitisha mkono na kugusa mgongoni.

Niliendelea kukipapasa papasa zaidi ili niweze kukifahamu.

“Anhaa!”, nilisema mara baada ya kuona kitu hicho kikifanana na begi la mgongoni.

Nilipapasa zaidi kwa upande wa kushoto chinichini kidogo ya begi hilo. Na mara nikaishika kamba fulani iliyokuwa imeegeshwa na kuning’inia pembeni mwa begi hilo.

FREE SAMPLE

“Just Pull It!”, nafsi yangu ilichangamka kuniambia.

Basi nilipoivuta, nilishangaa kuvutwa nyuma na kwa kasi ya ajabu sana kuelekea juu. Ni kama vile mtu akikushika shati na kukuvuta kwa ghafla uwapo kwenye mwendo.

Niligeuka nyuma na kutazama juu.

“Oh!”, Nilistaajabu sana kuona parachute kubwa la rangi ya orange, likiwa limenishikilia hapo hewani.

“Wow!”, nafsi ilishangilia.

Basi kifo kiliacha kabisa kutabasamu. Na mara moja kilitoweka na kuachana na mimi kwa siku hiyo ndani ya jiji la Dar.

Drone iliendelea kurekodi na kurusha moja kwa moja mtandaoni kila kile kilichokuwa kikiendelea. Na sasa ilikuwa inanirekodi namna nilivyokuwa nashuka chini taratibu kabisa kwa parachute hilo.

Kila mtu alianza kunishanga pale nilipokuwa naanza kutua chini kwa kuishusha miguu yangu kwenye ardhi. Wengi sana

FREE SAMPLE

walistaajabu kumuona mtu mwenye parachute akitua katikati ya jiji hilo la Dar.

Kilicho-wastaajabisha zaidi ni kumuona mtu mwenyewe akiwa amevalia mask usoni. Mask iliyoziba sura yake halisi.

Nakwambia, nilijikuta nimezingirwa na watu wengi sana. Kila mtu akiwa na simu yake aliyoiwasha Flashlight na Camera wakiwa wamezielekezea kwangu mimi. Ilionekana ni kitu cha ajabu mno kuwahi kutokea hapo katikati ya jiji, hususan kwa muda huo wa jioni yenye kuelekea usiku.

Basi hata madereva wa magari walijikuta wakisimamisha magari yao ili kuweza kujionea hicho kilichoweza kutua kwa parachute katika mkutano hayo ya barabara. Hii ilipelekea kusababisha foleni kubwa sana ya magari kama vile foleni ya madumu bombani pale maji yanapokatika kwa wiki nzima.

“Hii noma sasa”, nilijiambia mara baada ya kuona watu wakizidi kuongezeka eneo hilo. Mbaya zaidi hata polisi pia walipata taarifa na walishawasili eneo la tukio wakiwa na silaha zao kuhakikisha usalama zaidi wa eneo hilo la tukio.

“Oh!, my God”, nilijiambia mara bada ya kuona askari polisi

FREE SAMPLE

watatu wakiwa na Shot Guns. Walianza taratibu kunisogelea huku wakiniamuru kupiga magoti chini na ninyoshe mikono yangu juu.

“What should I do?”, niliiuliza nafsi yangu.

“Diss….!”, nafsi ilinipa jibu kwa kuninong’oneza.

Nilitazama kulia na kisha kushoto, mara pap! Nilijifunika chap chap kwa lile parachute. Kisha tuli! Nilitulia kimya kama kuku mwenye kulalia mayai yake.

Bada ya sekunde kadhaa, askari waliweza kulizingira lile parachute. Lakini walipolinyanyua na kulifunua, walibaki wakijiuliza swali moja tu!.

“YUKO WAPI?”, kila askari alijikuta akimuuliza mwenzie.

Kwa sababu, hawakuweza kuamini kabisa kile kilichoweza kutokea mbele ya poopoo zao mbili zivukazo mto.

Ukweli ni kwamba nilishawachoropoka na ku-disappear, yani nilitoweka, niliyayuka , ama ukipenda unaweza ukasema nilipotea kwa kutatanisha.

FREE SAMPLE

Sio wewe tu unayejiuliza kuhusu HOW DID I DISAPPEAR?. Nasema sio wewe peke yako bali hata wale polisi walibaki wakijiuliza hivyohivyo. Walishangaa, iliwashangaza na nilionekana ni mtu mwenye kushangaza mno.

“Huu ni uchawi huu!!”, mara zilisikika kelele za raia waliokuwa wamekusanyika eneo hilo la tukio.

“Haa! aa! Haiwezekani”, mara aliropoka mtu mwingine. Basi kila mtu alisema lile alilojisikia kulisema.

Askari waliongeza kikosi kingine zaidi na kulizungushia eneo hilo kwa kuliweka chini ya ulinzi na kwa ajili ya uchunguzi zaidi. Baadhi ya polisi wapelelezi waliendelea kupeleleza eneo hilo kwa kuangalia vitu kama vile footprints, finger-prints, pamoja na kuchora michoro ku-trace mpangilio wa vitu katika eneo hilo la tukio. Hasa hasa walichora namna parachute lilivyotua pale chini.

Maofisa wengine wa upelelezi waliendelea na kupiga picha objects mbalimbali zilizopo katika eneo la tukio kwa ajili ya Further investigation.

FREE SAMPLE

Punde si punde waandishi wa habari nao waliweza kuwasili eneo la tukio wakitokea katika vituo mbalimbali vya utangazaji hapa nchini. Wanawasili ndani ya eneo la tukio lililokuwa limezungushiwa kwa utepe wa njano ulio na maandishi yanayosomeka “CRIME ZONE!”.

Na sasa usiku ulishaingia huku kigiza kikianza kufunika anga kama vile kizee anapojifunika koti pale anapohisi baridi kali mwilini.

Mataa yenye mwanga mkali sana yaliwashwa kulizunguka na kulimulika eneo hilo la tukio. Pia polisi walioshikilia mitutu ya bunduki walisimama imara kuhakikisha usalama wa eneo hilo.

Basi waandishi wa habari waliendelea kuwahoji na kuwauliza maswali mbalimbali wale raia waliokuwa wamezunguka na kulishuhudia tukio hilo pale lilipokuwa likitokea.

Ndani ya muda mchache tu!, hali ikawa hali. Karibia kila stesheni ya runinga ilikuwa ikirusha “HABARI ZILIZOTUFIKIA HIVI PUNDE” yaani, “BREAKING NEWS”. Huku ikipamba habari hiyo kwa kusema…… “ATUA KWA PARASHUTI NA KUTOWEKA KWA KUTATANISHA”.

FREE SAMPLE

Nakwambia hadi barabara zilifungwa, yani zile zenye kuelekea kwenye makutano hayo ya eneo la tukio. Badala yake ilielekezwa njia nyingine ya kuweza kupita magari hayo yaliyokuwa yakielelekea sehemu mbalimbali za ndani na nje ya jiji la Dar es salaam.

Dakika thelathini baadae nilianza kuhisi maumivu makali mno kwenye maeneo ya kiunoni. Mapafu yalinibana na kupumua kwa shida sana. Miguu pia ilionekana kukosa nguvu. Na hata nilipojaribu kufumbua macho yangu sikuona chochote kile zaidi ya kigizagiza flani hivi.

Hapo ndipo niliamua kuivua ile mask niliyokuwa nimeivaa. Kisha niliangaza angaza sehemu iliyonizunguka ili kuifahamu.

Mara nilianza kuhisi harufu kali sana kama ya kuoza oza kwa vitu ikizitesa pua zangu.

“Ni wapi hapa?”, nilijiuliza huku nikigeuka nyuma. Hapo nikayaona matobo sita yaliyoweza kupenyeza miale michache ya mwanga. Lakini kabla sijakaa vizuri kutazama kwa nje, nilishangaa kuona sehemu ya juu ikifunguliwa.

FREE SAMPLE

"Kulikoni?!!", nilibaki najiuliza.

Mara kidogo tena nilishangaa kuona takataka zikimiminwa na kuniangukia mimi niliyemo humo ndani.

"Oh My God!", nilijishangaa sana kujikuta ndani ya………….

---

MWENDELEZO WA HADITHI HII UPO, NA UNAPATIKANA KWA GHARAMA NDOGO SANA YA SHILINGI ELFU NNE TU!.


ILA KUNA HII OFFER SASA, UNAWEZA KUPATA MWENDELEZO

**KWA SHILINGI 2000 TU!.**

**Tuma neno, "YUKO WAPI", kwenda wasap namba**

**0682 458 163**

**Kwa maelezo zaidi ya kuupata mwendelezo.**

SAMPLE